

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TANO

22 APRILI, 2021



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 22 APRILI, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **124. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Kituo cha Afya cha Kinesi kitapandishwa hadhi na kuwa Hospitali kamili kutokana na Kituo hicho kuhudumia zaidi ya Vijiji 27 katika Jimbo la Rorya.

#### **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

##### **125. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

- (a) Je, kwa nini barabara ya Mpanda – Ulyankulu – Kahama haikujengwa katika kipindi cha 2015 – 2020 kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020;
- (b) Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hiyo utaanza kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025.

## **WIZARA YA KILIMO:**

- 126. MHESHIMIWA MARIAM DITOPILE  
MZUZURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wakulima nchini kuwekeza katika kilimo cha mazao ya Alizeti, Michikichi na Karanga ili kuokoa kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi.



## **WIZARA YA NISHATI:**

- 127. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON  
RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini umeme utapelekwa katika Vijiji vya Buzi, Buguruka, Musina, Nsheshe na vingine ambavyo havijafikiwa na umeme katika Jimbo la Bukoba Vijijini.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

- 128. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA  
KITANDULA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itafanya zoezi la kuhakiki na kuweka alama kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya kwa eneo la nchi kavu na baharini ili Wananchi wa mpakani Wilayani Mkinga waondokane na kero ya muda mrefu ya kukamatwa na kutaifishiwa mali zao na Askari wa Kenya.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

#### **V. HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:**

SAA 10:00 ALASIRI.

**DODOMA  
22 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**